102/1
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
Julai/Agosti - 2015
**MUDA: SAA 1 ¾**

# MTIHANI WA KUTATHIMINI WILAYA YA BONDO - 2015
## *Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)*

102/1
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
Julai/Agosti- 2015
**MUDA: SAA 1 ¾ Hours**
MAAGIZO
1. Andika insha mbili
2. insha ya kwanza ni ya **Lazima**.
3. kisha chagua insha nyingine moja kutoka kwa tatu zilizosalia.
4. kila insha isipungue **maneno 400**.
5. kila insha ina **alama 20**.

Karatasi hii ina kurasa 2 zilizopigwa chapa.watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yalioachwa.

1. Wewe ni katibu wa kamati ambayo imeteuliwa na mkuu wa wilaya kuchugunguza chanzo cha mgomo wa wafanyakazi.Andika ripoti ya uchunguzi wa kamati hiyo.
2. Zindiko la mwoga ni kemi.
3. Vijana wa kiume wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kimaisha.Fafanua huku ukipendekeza hatua zifaazo kuchukuliwa ili kuzikabili changamoto hizo.
4. Saa tatu asubuhi ilinipata ndani ya Afisi ya mwalimu mkuu.Ilikua ni siku moja tu baada ya matokeo ya mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne kutangazwa, Bi Tumbo alinitazama kwa macho ya huruma.Alichotamka kilitafuna maini yangu.kijasho chembamba kikanipita,wosia wa aliyekua mwalimu wetu wa darasa kuhusu udanganyifu katika mtihani ukarejea kwa akili yangu………………………………………………………..(Endeleza)

www.eeducationgroup.com

**Jina…………………………………………………….Nambari yako……………………………**
**Shule…………………………………………………..Tarehe……………………………………**
**Sahihi yako…………………………………………….**

102/2
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**MUDA: SAA 2 ½**
Julai/Agosti - 2015

# MTIHANI WA KUTATHIMINI WILAYA YA BONDO - 2015
## *Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)*

102/2
**KISWAHILI**
**Karatasi ya2**
**MUDA: SAA 2 ½**
Julai/Agosti- 2015

**MAAGIZO**
Jibu maswali yote katika nafasi ulizoachiwa.

| | SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|---|
| 1 | Ufahamu | 15 | |
| 2 | Ufupisho | 15 | |
| 3 | Matumizi ya Lugha | 40 | |
| 4 | Isimu- Jamii | 10 | |
| | **Jumla** | **80** | |

Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yalioachwa

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali. (ALAMA 15)**

Ardhi ni mali ya taifa. Hivyo inampasa kila raia kuinafidhi. Hiii na *maana* kwamba hatuna budi kuwarithisha wana na wajukuu, vitukuu na vilembwe, vining'ina na wapwa zetu ardhi yenye rutuba. Ardhi ndiyo chanzo cha riziki zote. Fauka ya hayo, ardhi ni dafina kubwa.

Tangu asili ardhi hii ilikuwa imefunikwa na joho la miti na majani. Rutuba ilienea kila mahali. Lakini wakati ulifika ambapo wanadamu hawakuvumilia kukaa bila kuitumia johari hii. Walishika maparange na mashoka. Wakafyeka majani na miti yote. Wakalima wakapanda na kuvuna. Kisha walihama hapo. Waliendelea kufanya hivyo mwaka hadi mwaka. hali ya kufyeka sehemu mbalimbali za nchi, kuchoma mioto ovyo, kuwa na mifugo mingi na kutojua kuhifadhi ardhi vizuri kulileta mavuno hafifu kila mwaka.

Mvua iliponyesha matone ya mvua yaligonga ardhi. Maji yakajiri kwa nguvu na kutawanya chembe za udongo. Wakati wa kiangazi udongo ulipokauka, upepo mkali ulichukua tabaka la juu la ardhi na kueneza biwi la ghubari kila mahali. Udongo wa rutuba, ukawa umepotea kabisa. Hivyo ikawa mazao hayawezi kustawi. Hatimaye nchi ikawa kama mkuranga. Mambo haya yakasababisha mmomonyoko wa juu juu halafu mwanzo wa michirizi na mwisho makorongo na maporomoko ya ardhi.

Walakini basi ya kale hayapo. Sasa wakuu wa serikali yetu ya Insafu wamekuhimizeni, ikiwa mu wakulima, mpande zaidi. Wamewashaurini namna ya kuongeza mavuno katika mashamba yenu kwa maarifa bora ya zaraa, kama vile kuunafidhi udongo, kutumia mbolea, njia za kunyunyizia dawa makondeni ili kuua wadudu wanaoharibu mimea, na kutumia maarifa malihi katika kupanda mbegu. Kwa wale ambao si wakulima, serikali yetu ya Insafu imeweka shule za mafundisho maalum na kumhimiza kila mmoja wao aongeze maarifa yake na afanye kazi kwa tabasuri na bidii ili aongeze mapato yake na mapato ya serikali pia. Katika sehemu nyingine maelezo ya wakuu wa serikali yamefuatwa barabara, na kumetokea maongezeko malihi ya mazao.

Walakini pia katika sehemu hizo maongezeko yake hayakutosha sana. Katika sehemu nyingine kwa bahati mbaya watu wamepotezwa na watu wakaidi ambao kwa kutaka ushaufu, wamewaambia watu kuwa kuna njia rahisi na nyepesi ya kujipatia serikali ya kujitawala yenyewe, na wamewashawishi na kuwatisha baadhi ya watu waasi amri za serikali zihusuzo zaraa. Wahaini hao wametibua mambo. Ni watu wa kuaili na ni afkani.

**Maswali**

a) Toa sababu iliyowafanya watu wa kale kuhamahama kila rnwaka. (alama2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………

b) “Mifugo wengi wana hasara.” Fafanua kwa mujibu wa kifungu. (Alama3)

……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………

c) Ili kuzuia mmomonyoko wa udongo, ni hatua zipi zafaa kuchukuliwa? (Alama 5)

……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………

d) Huku ukitoa mifano, tathmini utendakazi wa wakuu wa serikali ya Insafu (Alama3)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

e) Eleza maana ya

i) Afkani

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

ii) Biwi Ia ghubari.

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

(Alama 2)

## MUHTASARI (ALAMA 15)

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Chonde pulika nikuelezeni juu ya maendeleo ya visiwa vya kwetu. Katika kisiwa cha Migingo wanaishi pamoja katika vijiji. Walianzisha vijiji hivi kwa ajili ya kuondoa dhuluma na dhiki ya mambo mengi ya lazima kwa maisha bora na ustawi. Wanaishi kwajasho lao. Ushirikiano ndio ngao ya msingi wa maendeleo. Watu wote wa kilajanibu na katika vitongoji vya kisiwa kizima ni kama ndugu. wanaishi kwa umoja. Ubaguzi umekwisha zikwa katika kaburi la sahau. Wote wanapenda kazi zao uvuvi. Hakuna anayepiga zohali. Ni aibu kwa kila rnwanakijiji kulaza damiu. Shibe ndiyo ngao yao kila mmoja anapigana kwa jino na ukucha kujaribu kuondoa hali ya unyonge, ufukara, ukosefu na hasa kuleta haraka iwezekanavyo hali ya maendeleo na ustawi kwa ashabu na kisiwa cha Migingo.

Viongozi na hata wazee wa vijiji hawaingii sana vijiji hivi hata ikiwa kuna tatizo kubwa. Hata hivyo viongozi wa serikali wanaangalia kama watu wote wanapata chakula bora na hasa watoto, kunywa maji safi ili kuepukana na magonjwa, kutoa huduma kwa akina mama, watoto na kuchukua hatua kadhaa za kuendeleza afya ya watu kwa jumla. Watu wa Msalaba Mwekundu husaidia mambo kadhaa na Mabwana Afya hushughulika kuzuia magonjwa ya kuambukiza kwa njia ya kuchanja kama vile ndui, kipindupindu na kadhalika.

Watawala wa Migingo wanatilia mkazo kwa watu wazima kuimarisha uvuvi ambao ndio uti wa mgongo wa kisiwa hiki ili kuinua hali ya uvuvi, uchumi na maendeleo ya kisiwa kwa ujumla.

**Maswali.**

a) Fupisha aya ya kwanza kwa maneno 50. (Alama 6, 1 utiririko)
Matayarisho

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

Jibu

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

b) Bila kupoteza maana asilia, andika mambo yote muhimu kutoka aya mbili *za* mwisho.
(Maneno 60) (Mama 7, Utiririko I)

Matayarisho

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

Jibu

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

3. **SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA. (ALAMA 40)**

a) Ainisha mofimu katika neno 'Tunacheza'. (Alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

(b) Vitenzi vifuatavyo ni vya aina gani. (Alama 2)

Wewe ndiwe mchokozi.

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

Mwanafunzi aliyecheza vizuri ametuzwa.

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

(c) Tunga sentensi yenye:

(i) Changizo ya mahali

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

(ii) Kiunganishi <u>wala</u> (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(d) Nomino katika ngali ya U – ZI huchukua maumbo tofauti katika umoja na wingi.Tetea kauli hii kwa mifano yoyote minne. (Alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(e) Nywele zao zilinyolewa zote.Andika kwa umoja. (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(f) Tofautisha kati ya

(i) Mwenye macho haambiwi ona.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(ii) Mwenyewe haambiwi ona.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(Alama 2)

(g) Weka vitenzi hivi katika kauli ya kutendesha.

(i) Lewa

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(ii) La

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(Alama 2)

(h) Changanua sentensi hii kwa kielezo cha mchoro matawi. (Alama 4)

Kiti kilichonunuliwa na mama jana kimekaliwa bwenini.

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(i) Mama alisema kuwa atamlimia afurahi ndipo amlipe vizuri. (Tambua sentensi sahihi zilizoko katika sentensi hii) (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

j) Toa maana mbili za sentensi hii.

Aliliulia lake. (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

k) Kangumu alisema "Masomo yetu yatakuwa rahisi rnwaka huu hivyo hatutaumia sana."
Geuza kwa usemi wa taarifa. (Alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

l) Alitembea na maringo alipokuwa ako mle kwao. Sahihisha. (Alama 3)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

m) Weka shadda katika neno ‘MBONO’ ili kuleta maana tofauti. (Alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

n) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiimbo. (Alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

o) Eleza matumizi yoyote mawili ya parandesi. (Alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

p) Kanusha. (Alama 2)

i) Naimba nikilia

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

ii) Amekuja tena

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

q) Weka nomino katika ngeli zao. (Alama 2)

i) Kitwana

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

ii) Maradhi

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

Maajuzi "wasee" wa TLB walipiga kambi kwenye "rodi"ya kwetu. Walikuwa pamoja na "makarao" na "makadigo."Wacha "wasakanye" "madinga". Kusikia hivyo ilibidi tupige "sosa" na "inga" letu likachania mbugani.

a) Hii ni sajili gani? (Alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

b) Taja sifa zozote sita za sajili hiyo. (Alama 6)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

c) Toa sababu tatu za kuzuka kwa sajili hiyo. (Alama 3)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

*Mwisho*

102/3
**KISWAHILI**
**Karatasi ya3**
**Fasihi**
Julai/Agosti - 2015
**MUDA: SAA 2 ½**

# MTIHANI WA KUTATHIMINI WILAYA YA BONDO - 2015
***Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari (K.C.S.E)***

102/3
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**
**Fasihi**
Julai/Agosti- 2015
**MUDA: SAA 2 ½**

**MAAGIZO**
1. Jibu maswali MANNE pekee.
2. Swalii la kwanza ni la lazima.
3. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki,yaani:Tamthilia,Riwaya,Hadithi fupi na fasihi similizi.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
5. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za Karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa yote yamo.

*Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa.*

*watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yalioachwa.*

**SEHEMU YA A: USHAHIRI**

1. **SHAIRI 'A'**

(i)
Umekata mti mtima
Umeangukia nyumba yako
Umeziba mto hasira
Nyumba yako sasa mafurikoni
Na utahama
Watoto wakukimbilia

(ii)
Mbuzi kumkaribia chui
Alijigeuza panya
Akalia kulikuwa na paka
Kichwani
Mchawi kutaka sama kutisha
Alijigeuza samba
Akalia na risasi kichwani

(iii)
Jongoo wapi sasa yatakwenda
Bwanako kumpa sumu?
Hadija umeshika nyoka kwa mkia
Hadija umepitia nyuma ya punda
Jogoo kataka sana kukimbia
Aliomba miguu elfu

(iv)
Akaachwa na nyoka
Hadija wapi sasa
Bwanako kumpa sumu?
Hadija umashika nyoka kwa mkia
Hadija amepita nyuma ya punda

**SHAIRI 'B'**

Piteni jamani,piteni haraka
Nendeni ,nendeni huko mwendako
Mimi haraka, haraka sina
Mzigo wangu,mzigo mzito mno
Na chui sitaki kuweka

Vijana kwa nini hampiti?
Kwa nini mwanicheka kisogo?
Mzigo niliobeba haupo.

Lakini umenipinda mgongo na
Nendako
Haya piteni!piteni haraka!Heei!

Mwafikiri mwaniacha nyuma!
Njia ya maisha ni moja tu.
Huko mwendako ndiko nilikotoka
Na nilipofikia wengi wenu
Hawatafika

Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati
Lakini kama mungepita mbele
Na uso wangu kutazama
Ningemwambia siri ya miaka
Mingi

**Maswali**

(a) Haya ni mashairi ya aina gani?Toa sababu. (Alama 2)
(b) Washairi hawa wawili wanalalamika.Yafafanue malalamishi yao. (Alama 4)
(c) Onyesha jinsi kinaya kinavyotokeza katika tungo hizi mbili. (Alama4)
(d) Ni vipi Hadija :-
  (i) Amekata mti mtima? (Alama 2)
  (ii) Amepita nyuma ya punda. (Alama 2)
(e) Toa mifano miwili ya uhuru mshairi kwa kurejelea mashairi haya. (Alama 2)
(f) kwa kurejelea shairi 'B' eleza maana ya:-
  (i) Mzigo
  (ii) Siri
  (iii) Kula nimekula
  (iv) Niko nyuma ya wakati. (Alama 4)

**SEHEMU YA B: RIWAYA – UTENGANO na Said A. Mohamed**

2. "Leo amekomolewa na bado ataumwa na nge kwa mdomoni na mkiani".
   (a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (Alama 4)
   (b) Eleza kwa kutoa hoja nane jinsi anayerejelewa alivyoumwa na nge. (Alama 8)
   (c) Eleza sifa nne za mnenaji. (Alama 8)

3. Mkamia maji yanywi,akiyanywa humsakama.Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea wahusika wowote watano katika Riwaya ya Utengano. (Alama 20)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA – MSHTAHIKI MEYA – Timothy M. Arege**

4. ……………………. Fimbo ya meya ipo?
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
   (b) Eleza wahusika wa muktadha huu walikua na azma gani katika mazungumzo yao. (Alama 6)
   (c) Taja mifano yoyote ya miovu iliyotokea katika mchezo huu inayohujumu Maendeleo katika muktadha huu. (alama 12)

5. Orodhesha huku ukitoa ushahidi masaibu yaliyowakumba wamacheneo. (Alama 20)

**SEHEMU YA D: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

6. "leo ni siku ya siku ,siku ya nyani kufa na ambapo miti yote huteleza."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
   (b) Tamathali zipi za usemi zimetumika katika dondoo na kwa dhima gani? (Alama 6)
   (c) Eleza sifa zozote tano za mhusika anayehusishwa na dondoo hili. (Alama10)

7. Linganisha na ulinganue maudhui ya ushirikina katika hadithi ya Gilasi ya mwisho makaburini na hadithi ya kikaza. (Alama 20)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8. (a) Taja sifa tanzu zifuatazo za fasihi simulizi.
      (i) Hurafa (Alama 2)
      (ii) Mighani (Alama)
      (iii) Miviga (Alama 2)
   (b) Eleza umuhimu wa ngomezi katika jamu. (Alama 6)
   (c) Eleza sifa nne za mafumbo. (Alama 4)
   (d) Eleza tofauti mbili kati ya malumbano ya utani na mawaidha. (Alama 4)